# Menejimenti ya kodi yaleta kiwingu ukuaji ujasiriamali



Ofisa Mtendaji wa Sekta Binafsi nchini (TSPF), Godfrey Simbeye.

Na Beda Msimbe

TATHMINI iliyofanywa na sekta binafsi mwaka 2012 kwa kuangalia sera za kodi za serikali na kiwango cha juu cha kodi kinachopotea kutokana na ukwepaji inaonesha kwamba taasisi mbalimbali huripoti asilimia 69 tu ya mauzo yao na kwamba taasisi zisizo rasmi hazilipi kodi kwa takriban asilimia 40.

Kwa ujumla, ripoti hiyo inayofanya sehemu ya chapisho la Mtazamo wa Viongozi wa Biashara kuhusu Mazingira ya Uwekezaji Tanzania, inaonesha kwamba serikali hukusanya kiasi cha dola za Marekani bilioni 1.3 kwa mwaka kiasi ambacho dhahiri ni kidogo mno. Kiasi hicho kimsingi ni sawa na moja ya sita ya bajeti ya serikali.

Ofisa Mtendaji wa Sekta Binafsi nchini (TSPF), Godfrey Simbeye, anasema ipo haja ya kurahisisha mfumo wa kodi na kuongeza uwazi katika ukusanyaji sanjari na matumizi ya serikali.

Katika majadiliano hivi karibuni wakati wa kuzindua ripoti hiyo, wachangia mada na watu waliopewa kuzungumza walitaja tatizo la menejimenti ya kodi, kanuni na sheria zake kama kikwazo kikubwa cha uwekezaji na hivyo kudidimiza biashara nchini.

Kwa mtazamo wa viongozi wa biashara, menejimenti ya kodi Tanzania ni kero.

Katika moja ya nyaraka za walipa kodi zilizofika katika ofisi za gazeti hili, mtu ambaye alijitambulisha kwa jina lisilo rasmi kama "truth war" anayepatikana katika mtandao wa komyuta duniani kama truth10@outlook.com alilalamika vikali kuhusu mazingira ya ulipaji kodi.

Aliliambia gazeti hili kwamba kuna vurumai kubwa ndani ya Mamlaka ya Mapato kuhusu kodi, mashine na hata tozo nyingine ambazo zinaonekana kumkimbiza mfanyabiashara kutumiza wajibu wake kwa taifa, kwenye ulipaji kodi. Kwa namna ya pekee, mfanyabiashara huyo ambaye alidai kuwa anazungumza kwa maslahi ya taifa anasema kwamba watu wengi wanakwepa kulipa kodi kutokana na mizozo isiyokuwa na msingi inayoambatana na mfumo mzima wa kodi na tozo nchini.

Anasema pamoja na anaoita ubabe wa maofisa wa Mamlaka ya Mapato (TRA) kuvamia ofisi na kunyakua vitabu vya risiti pia kuna shida ya kulazimishwa kununua mashine za kukatia risiti za kielektroniki na kusema huo ni mzigo mkubwa kwa wafanyabiashara.

Aidha anasema hata katika kusafirisha bidhaa zao wanakumbana na vikwazo ambavyo si vya lazima na kusema kwamba serikali ni lazima iangalie nini cha kufanya kuondokana na mizgo huu.

Wengi wa watu waliohojiwa kwa njia ya simu na mwandishi wa makala haya wamesema pamoja na nia njema ya kuzuia wakwepa kodi lakini menejimenti ya kanuni na sheria haiko sawa, ni kama vile kuna msuguano wa kijambazi kati ya serikali na walipa kodi wake.

Pamoja na ukweli kuwa mashine hizo ni gharama kubwa lakini kitendo cha serikali kuwataka wafanyabiashara ndio wazinunue kinaonekana si cha haki.

Katika mazingira yaliyopo ni dhahiri kwamba rushwa huenda ikaota mizizi katika kusukumana huku. Katika utafiti uliofanywa na Sekta Binafsi nchini kuhusu mazingira ya uwekezaji na ripoti yake kuzinduliwa hivi karibuni katika jengo la Karimjee, shauri la menejimenti ya kodi ndilo lililotawala mjadala.

Katika ripoti hiyo watu wengi waliohojiwa kuhusu vikwazo vya kutolipa kodi walisema wazi kwamba mazingira yapo magumu, kodi kubwa, kuvutana na kutoelimishana kuhusu kodi hizo na hasa wale ambao wana maeneo mengi ya kuchukulia leseni na malipo maeneo tofauti tofauti.

Ofisa Mtendaji wa Chama cha Wafanyabiashara, Wenye Viwanda na Kilimo mkoani Dodoma (TCCIA), Fred Azaria anasema kwamba mfumo wa ulipaji kodi wa Mamlaka ya Mapato ni mzuri kutokana na kugawa makundi ya biashara kulingana na ukubwa wake katika kila eneo.

Lakini pia alizungumzia makundi yanayokimbia kulipa kodi na kusema kwamba yanahitaji kuelimishwa.

Katika mahojiano kama kweli anaridhika na mfumo wa ulipaji, ofisa huyo wa TCCIA alisema ulipaji wa kodi ya ongezeko la thamani (VAT) unaofanywa na wafanyabiashara wenye mzunguko unaozidi Sh milioni 40 na kodi ya mapato vimewapa wafanyabiashara nafasi ya kujikadiria kodi.

Anasema wafanyabiashara wenye mzunguko unaozidi milioni 40 kisheria wanatakiwa kujisajili ndani ya siku 30 na TRA imeanzisha utaratibu kwa kuweka mashine za kielektroniki za kundi hili kwa lengo la kutathimini mahitaji ya soko.

Anasema changamoto kubwa ni wafanyabiashara kuelewa watakavyojikadiria na endapo mtu amekadiria kiwango cha chini atatakiwa kulipa tofauti iliyopo.

**Mfumo wa ulipaji kodi**

Pamoja na watu wengi katika mkutano wa hivi karibuni wa Karimjee kuona mfumo wa ulipaji kodi una walakini, ofisa mtendaji wa Dodoma wa TCCIA anasema ni mzuri hasa katika suala la ukusanyaji wa mapato. Anasema kumekuwa na uwazi na kwamba walipa kodi wamepewa nafasi ya kujikadiria na kujitetea hasa pale wanapoona hawakutendewa haki.

Hata hivyo, anasema kwamba tatizo kubwa ni utekelezaji wa sheria kwani jinsi ilivyo sheria haizingatii mfumo wa kodi.

Anasema kwa upande wa Dodoma, TCCIA inandaa utaratibu wa kuwafikia wafanyabiashara ili waweze kusajili biashara kutokana na kuwepo kwa wimbi kubwa la biashara zisizosajiliwa ambazo hazitambuliki kisheria.

Anasema TCCIA kwa kushirikiana na Mamlaka ya Usajili wa Biashara (BRELA) imeandaa utaratibu wa kuwataka wafanyabiashara kufika TCCIA kwa ajili ya kuunganishwa ili waweze kupata usajili wa biashara zao na kwa namna hiyo kutambulika kuwa ni walipa kodi.

Anasema pia kwa sasa kuna wimbi kubwa la biashara ambazo hazijasajiliwa na hazilipiwi kodi, jambo ambalo linasababisha hata masuala ya elimu ya biashara kuwa vigumu kuwafikia.

Anazitaja miongoni mwa biashara hizo kuwa ni zile za vyakula zinazoendeshwa na mama lishe na hata biashara za maduka yaliyopo mitaani ambayo mengi huendeshwa bila kuwa na usajili.

"Wafanyabiashara wengi hawana leseni na wamekuwa wakifanya biashara kiholela. Lengo lililopo sasa ni kuwasajili ili waweze kulipa kodi na ili waweze kutambulika kisheria na kufanya shughuli zao kihalali. Jambo hilo linaweza kuwasaidia kupata mikopo kwenye taasisi za kifedha na hata kupata elimu mbalimbali juu ya biashara," anasema. Mwenyekiti wa Rulu Arts Promoters, Angelo Luhaha, anasema yeye anaona kuna hitilafu kubwa sana katika menejimenti ya kodi nchini Tanzania.

Anasema pamoja na ukweli kuwa tozo zipo nyingi katika kila biashara unayotaka kuifanya ukiachia mbali kodi ya serikali kuu, lakini mfumo wa kodi Tanzania na aina yenyewe za kodi haupo sawasawa.

Katika mahojiano ya simu anasema yeye anakerwa na mambo makubwa matatu kwa sasa. Moja ya mambo hayo anasema ni tabia anazoita za kibabe za maofisa wa TRA, mzigo wa ununuzi wa mashine za kodi na tozo zinazokwamisha maendeleo ya watu wa hali ya chini. Pia anaelezwa kukerwa na tozo ya simu ambayo ndio msingi wa mawasiliano ya watu wa mjini na vijijini katika biashara.

Anasema ipo haja kwa TRA kusikiliza watu wanasemaje kuhusu kodi wanazotoza ili isiwe mzigo mzito kwa watu wengine huku mamlaka mbalimbali nchini zikiangalia tozo zao zisimmalize mfanyabiashara.

Mathalani anasema kodi ya ongezeko la thamani ambayo ni asilimia 18 ni ya juu sana huku matumizi ya mashine za kielektroniki yakiwa yanamkamua zaidi mfanyabiashara.

"Tabia ya kumpa mfanyabiashara zigo la kununua mashine hizi badala ya TRA kunawaumiza wafanyabiashara na hakuna sababu," anasema Luhaha na kuongeza kwamba serikali yenyewe lazima iweke miundombinu na wengine watumie miundombinu hiyo kukidhi haja ya taifa.

Anahoji: "Mfanyabiashara wa kawaida atapata wapi laki nane ya kununulia mashine ili kuiwezesha serikali kukusanya mapato yake? Huko ni kuwaonea wafanyabiashara na kuwafanya wawe watu wa kubuni namna ya kujinasua," anasema.

Anasema ukusanyaji wa ushuru na tozo kutoka kila mahali na hata kwenye simu kunapunguza vile vile uhakika wa ulipaji kodi kwa kuwa mtu anakamuliwa kila mahali. "Tulikuwa tunatumia sh 450 kupata huduma ya Mini Kabang katika simu za Tigo kwa mfano, sasa ni sh 600. Watu wa vijijini wataweza kweli?" anazidi kuhoji.

Aidha anaitaka Mamlaka ya Kodi kuangalia namna ya kuwatumia wafanyakazi wake na kuwa na tabia njema na si kuvamia maeneo ya kazi kila siku na kuanzisha usumbufu.

Kuhusu mashine za kielektroniki, pamoja na ughali wake watu wa TCCIA- Morogoro kwa ufadhili wa BEST AC walifanya utafiti uliobainisha kwamba baadhi ya mashine hizo zina matatizo ya mtandao. Lingine walilolalamikia ni ughali wake na kusema badala ya kupunguza kazi inawaongezea maumivu hasa inapotokea kwamba ni lazima kupeleka fedha lakini mtandao haupo.

Aidha walisema kulikuwa hakuna mfumo wa uagizaji wa mashine hizo na hivyo bidhaa hafifu kuingia na kuwaletea shida kubwa wafanyabiashara ambao nao huduma za kifundi walilazimkika kuzifuata kwa umbali mrefu.

Wote wanasema, pamoja na nia njema ya serikali, sekta binafsi imekuwa ikikwazwa na mfumo mbovu wa menejimenti ya kodi.